KANDA YA ZIWA



# Kilio cha tozo chahamia kwa wavuvi

**Ni kuhusu ushuru mpya wa asilimia 2 ya samaki wanaouzwa viwandani, wakumbushia machungu ya Operesheni Sangara**

Saada Amir, Mwananchi
samir@mwananchi.co.tz



Baadhi ya wavuvi katika mwalo la Mswahili jijini Mwanza wakiandaa vyombo vyao tayari kwend kuvua ndani ya Ziwa Victoria. **Picha na Saada Amir**

Baada ya kilio cha tozo kwenye miamala ya fedha kupitia simu za mikononi ambacho kinaendelea kufanyiwa kazi, sauti mpya zimepazwa na wavuvi kuhusu tozo ya asilimia 2 kwenye mauzo ya samaki viwandani.

Vilio vya wavuvi kuhusu tozo hiyo mpya vinakuja wakati sekta ndogo ya uvuvi ikikabiliwa na changamoto kadhaa za muda mrefu ikiwemo tija ndogo, matumizi ya zana na teknolojia duni na wingi wa tozo nyingine za Serikali Kuu na halmashauri.

Miongoni mwa wizara zinazotoa leseni, vibali na tozo karibia 13 ni wizara mama ya Mifugo na Uvuvi, Tamisemi kupitia halmashauri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Fedha na Mipango pamoja na ile ya Viwanda na Biashara.

Tozo hiyo ya zuio la asilimia 2 kwa samaki wanaouzwa viwanda ni imeanza rasmi Julai Mosi katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali na kuibua malalamiko ya wavuvi na kusuasua kwa biashara hiyo.

Katibu wa Chama cha Wavuvi Tanzania (Tafu), Jephta Machandalo alisema tozo hiyo inatia chumvi kwenye kidonda cha wadau wa sekta ya uvuvi, ambao kwa muda mrefu wanakabiliwa na changamoto kadhaa, ikiwemo wingi na ukubwa tozo za awali.

"Tulitarajia Serikali ipunguze wingi na viwango vya tozo na kodi zilizokuwepo ili kuongeza tija kwenye sekta ya uvuvi badala ya kuanzisha tozo mpya.

"Wapo wanaodai asilimia 2 ni ndogo, lakini jambo wasilolijua ni kwamba tangu Julai Mosi, mvuvi anayeuza samaki wa Sh5 milioni kiwandani analipa Sh100, 000 (asilimia 2) na samaki wa Sh20 milioni analipa zaidi ya Sh400, 000, Hiki ni kiwango kikubwa cha fedha kinachoongezeka," alisema.

Mwenyekiti wa Tafu, Bakari Kadadi alisema kuanzishwa kwa tozo mpya ni mzigo mwingine kwa wadau wa sekta ya uvuvi ambao tayari wanalipa kodi na tozo 13 za Serikali kuu na nyingine za halmashauri.

Mvuvi na wakala wa kukusanya samaki kwa wavuvi, Winston Sebastian ni miongoni mwa walioonja joto la tozo mpya baada ya kujikuta akikatwa Sh500, 000 kutoka kwenye malipo yake ya kuuza kiwandani samaki wenye thamani ya Sh27 milioni.

"Mimi nalipa kodi kupitia makadirio ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), hivyo kitendo cha kukatwa Sh500, 000 na kuelezwa ni tozo kilinishangaza ikabidi niulize kwa viongozi, ndipo nikaambiwa kuna tozo mpya ya asilimia 2 imeanza. Sisi wenye namba ya TIN tunahisi tunatozwa kodi mara mbili kwenye bidhaa moja," alisema Sebastian.

**TOZO 13**

1. Kodi ya mapato kulingana na makadirio ya TRA.
2. Leseni za biashara katika halmashauri.
3. Ushuru wa kati ya Sh100 hadi Sh2,300 kwa kila kilo ya samaki inayonunuliwa
4. Leseni ya kukusanya na kusafirisha samaki.
5. Kibali cha ubora wa chombo cha kusafirishia.
6. Ushuru wa huduma.
7. Leseni ya kusafirisha samaki kutoka (Tasac).
8. Leseni ya usajili wa chombo kipya.
9. Leseni ya chombo inayoanzia dola 50 za Marekani na kuendelea.
10. Kodi ya asilimia 25 wakati wa ununuzi wa nyavu.
11. Kodi ya mapato ya mafuta ya vyombo vya uvuvi.
12. Ushuru wa maegesho ya vyombo vya uvuvi.
13. Uhuru wa vibali vya Kikosi cha Usimamizi wa Mialo (BMU).



Mwenyekiti wa Chama cha Wavuvi Tanzania (Tafu), Bakari Kadabi akipima uzito samaki aina ya Sangara katika mwalo wa Malehe Beach uliopo Bukoba vijijini mkoani Kagera. **Picha na Mpiga picha wetu**

Kilio cha tozo pia kimesikika kutoka kwa Moshi Mahonda, mvuvi katika Kisiwa cha Ghana, Wilaya ya Ukerewe aliyesema tozo mpya kinazidisha hali ngumu miongoni mwa wavuvi ambao hawajarejea katika hali nzuri kiuchumi baada ya madhara ya Operesheni Sangara iliyofanyika mwaka 2018 ikihusisha kukamata na kuteketeza zana haramu za uvuvi.

## Majibu ya Waziri

Akizungumza ma *Mwananchi* kwa njia ya simu mwishoni mwa wiki, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alisema Serikali inafanyia kazi changamoto zinazoikabili sekta ya uvuvi ikiwemo malalamiko kuhusu tozo hiyo.

"Kabla ya kuanzishwa kwa tozo hii, wadau wanaohusika walishirikishwa. Tatizo tunalokumbana nalo ni wavuvi kukosa chombo kimoja cha uwakilishi. Lakini Serikali imepokea na inafanyia kazi hoja zao," alisema Waziri Ndaki

Miongoni mwa maeneo yanayofanyiwa kazi na Serikali kwa mujibu wa Waziri Ndaki ni suala la idadi ya tozo na mtawanyiko wa idara, taasisi na mamlaka zinazosimamia sekta hiyo.

"Wizara ya Mifugo na Uvuvi ina tozo mbili pekee kwenye sekta ya uvuvi – tozo za leseni na ya royalty (mrabaha); lakini ukienda ngazi ya halmashauri utakuta karibia tozo 10. Tunashirikiana na wizara zingine ikiwemo Tamisemi kutatua changamoto ya wingi na viwango vya tozo," alisema Waziri Ndaki

Alisema kupitia mpango wa Blue print, Serikali si tu inalenga kupunguza wingi na viwango vya tozo, bali pia kuondoa urasimu mrefu kwenye biashara na uwekezaji katika sekta ya uvuvi kwa kuanzisha kituo kimoja kitakachohudumia wafanyabiashara na wadau wa sekta hiyo.

"Lengo la Serikali ni kuona watendaji wa sekta ya uvuvi wanapatikana chini ya mwamvuli mmoja na (one stop Center) nas hapo pawe na watendaji na viongozi wenye uwezo na mamlaka ya kufanya maamuzi kuondoa urasimu wa njoo kesho," alisema Waziri huyo.

Kadadi alisema wameanza mchakato wa majadiliano na Serikali kuhusu tozo mpya huku baadhi ya wavuvi na mawakala wa kukusanya na kuuza samaki wakiwa wamesitisha biashara kuepuka hasara.

Kutokana na uamuzi huo, baadhi ya wavuvi wameamua kuuza bidhaa zao katika soko la rejereja ambao nao huwauzia wafanyabiashara wadogo wakiwemo wa kukausha samaki kwa ajili ya masoko nje ya mkoa na wilaya za pembezoni.

"Tozo mpya zitasababisha viwanda vya samaki kufungwa, wafanyakazi kukosa ajira na hatimaye Serikali kukosa hata mapato ya sasa," alisema Kadadi.

Scanned with CamScanner

KITOWEO SALAMA

# Machinjio Vingunguti sasa rasmi

Mariam Mbwana na Bakari Kiango, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz




Mwonekano wa jengo la machinjio ya kisasa ya Vingunguti lililopo jijini Dar es Salaam. **Picha na Sunday George**

Dar es Salaam. Machinjio ya kisasa ya Vingunguti yameanza kufanyakazi baada ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuyabidhi Julai 29 kwa uongozi wa jiji.

Mwezi uliopita, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla aliitaka NHC kufanya kazi usiku na mchana ili Agosti mosi machinjio hayo yaanze kutumika.

Akizungumza na *Mwananchi*, Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto alisema machinjio yalianza kufanya kazi usiku wa kuamkia Julai 31 baada ya mkandarasi kuyakabidhi.

Kumbilamoto alisema kwa kuanzia uongozi wa jiji umetoa nafasi kwa wafanyabiashara kuchinja bure kwa siku tatu wakati utaratibu mwingine unaandaliwa.

"Baada ya hapo jiji litakutana na wadau hawa ili kuweka kiwango sahihi watakachotakiwa kulipia kwa ajili ya huduma ya kuchinja. Tunataka kuweka tozo ambazo hazitawaumiza wafanyabiashara hata watu binafsi watakaotaka huduma," alisema Kumbilamoto.

Meya huyo ambaye ni diwani wa Vingunguti alisema eneo la zamani la machinjio litatumika kama maegesho ya magari na wafanyabiashara watakaokwenda kufuata huduma za kuchinja pia kutajengwa mgahawa.

Alisema ndani ya wiki mbili wafanyabiashara wa machinjio ya zamani, watahamishiwa eneo la Mtakuja kwa ajili ya kufanya shughuli zao kwa ufanisi. Alisema eneo hilo limejengwa soko ambalo lipo katika hatua za mwisho kukamilika.

"Ukitaka nyama utakwenda Soko la Mtakuja siyo machinjioni tena. Machinjio ni kwa ajili ya kuchinja nyama ambazo zitakuwa bora zenye viwango vya kuuzwa katika masoko ya kimataifa," alisema Kumbilamoto.

Akizungumzia utaratibu wa kuchinja katika machinjio hayo mapya, Ofisa Mfawidhi wa machinjio hayo, Jabiri Ndabise alisema ili kuchinja, mchinjaji anapaswa kujiandikisha jina na idadi ya mifugo anayohitaji kuchinja kwa mfawidhi huyo.

"Utaratibu ni rahisi na rafiki kwa watu wanaotaka kupata huduma katika machinjio haya," alisema Ndabise.

Vilevile, kiongozi wa wafanyabiashara katika machinjio hayo, Joel Meshack alisema kuanza kufanya kazi kwa machinjio mpya kutawawezesha kukuza zaidi soko la nyama kutokana na kuongezeka kwa thamani.

"Hatukuwa tunaweza kupata nyama yenye ubora wa juu kuuza nje ya nchi lakini sasa machinjio mapya iyatatuongezea thamani ya nyama na mazao yatokanayo na wanyama wanaochinjwa hapa," alisema.

Mradi huo umegharimu Sh12.4 bilioni na utakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 1,500, mbuzi na kondoo zaidi ya 3,000 kwa siku kiasi ambacho ni kikubwa mara mbili zaidi ya machinjio ya zamani ambayo uwezo wake ulikuwa hadi ng'ombe 400. Vilevile, utatoa ajira zipatazo 3,000 kwa vijana na wanawake.

**MAPATO YA JIJI KUPAA**

**Kuanza kufanya kazi kwa machinjio ya Vingunguti kutaliwezesha Jiji la Dar es Salaam kukusanya kati ya Sh2 bilioni na Sh5 bilioni kwa mwaka zitakazoliwezesha kufanikisha gharama za uendeshaji pamoja na kutekeleza miradi mingine ya maendeleo.**

**Licha ya machinjio hayo jiji hili pia limejenga stendi mpya na linakamilisha daraja la baharini, miradi itakayotanua wigo wa mapato ya halmashauri.**

DC ao na bi

Mwan

## Tehama kutawala Sensa ya Watu na Makazi 2022

Na Yohana Shida, Geita

SENSA ya Sita ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika Oktoba mwakani, inatarajiwa kuhusisha zaidi matumizi ya vifaa vya teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehama) zikiwemo simu janja, vishikwambi na dadavuzi mpakato kwa mawakala wa sensa ili kuongeza usahihi wa takwimu.

Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kwa upande wa Tanzania Bara, Anna Makinda, alisema hayo akiwa ziarani Chato katika Mkoa Geita kukaguzi na kuangalia hali ya maandalizi ya utengaji wa maeneo ya sensa hiyo.

Alisema wakati wa sensa, wakala atajaza taarifa za kila familia anayopita moja kwa moja kwenye fomu maalumu ndani ya kishikwambi kisha taarifa kutumwa na kupokelewa papo hapo Ofisi Kuu ya Takwimu (NBS) hali itakayowezesha kupatikana kwa takwimu sahihi na kwa muda mfupi.

Alieleza kutakua na mfumo wa Tehama utakaosimamia, kufuatilia na kufanya utambuzi wa kila wakala kama takwimu alizojaza zinahusiana na eneo alipo ili kuzuia mawakala wasio waaminifu kujaza na kutuma taarifa za uongo bila kufika eneo husika.

Aliwaomba wakuu wa mikoa na wilaya kuwandaa

# Tanzania yajiandaa mkutano usalama wa chakula duniani

Na Mwandishi Wetu

MAANDALIZI ya Serikali ya Tanzania kushiriki mkutano ujao wa Umoja wa Mataifa wa Mifumo ya Usalama wa Chakula Duniani (UN 2021 Food System (Summit) yapo katika hatua nzuri.

Mpaka sasa mikutano 11 ya majadiliano 11 ya wadau mbalimbali katika sekta ya usalama wa chakula yiamefanyika ili kuandaa muhtasari wenye maazimio na ahadi za Tanzania utakaowasilishwa katika mkutano huo.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Kitengo cha Usalama wa Chakula nchini, Dk Honest Kessy ambaye pia anasimamia mikutano hiyo nchini.

Alisema katika siku za karibuni katika midahalo ya mwisho kuhusu mkutano huo wa Umoja wa Mataiofa utakaofanyika Septemba, wadau walifikia makubaliano kwamba ipo haja ya kuboresha mifumo inayohakikisha usalama wa upatikanaji wa chakula.

Katika mazungumzo hayo, ilibainika kwamba kunatakiwa uwekezaji mkubwa ili kuboresdha mfumo wa upatikanaji wa chakula kutokana na ukweli kuwa, Tanzania ni ghala la chakula kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati hasa upande wa nafaka, lakini huuza nafaka zake hizo zikiwa ghafi.

Majadiliano na mikutano hiyo iliyofanyika katika mikoa kadhaa Tanzania Bara na Zanzibar yalihusisha sekta binafsi, sekta ya umma na mashirika yasiyo ya kiserikali yamelenga kuwa na msimamo mmoja wa uwasilishaji wa taarifa katika mkutano huo utakaofanyika Septemba mwaka huu.

Meneja wa AGRA Tanzania, Vianey Rweyendela, alisema takwimu zilizopo zinaonesha Tanzania inafanya mabadiliko makubwa katika kilimo.

«Huku nchi ikiwa inajitosheleza kwa chakula kwa miaka mingi sasa, muda umefika kwa ziada hiyo kutumika katika kuleta mapinduziya viwanda na biashaera ili kusaidia wakulima wadogo,» alisema Rweyendela.

Mbunge wa Viti Maalumu Neema Lugangira, akiwasilisha asasi zisizo za kiserikali katika moja ya mikutano, alitaka kuongezwa kwa mchango wa kilimo katika pato la taifa.

Lugangira alisema ipo haja kufanyika kwa mabadiliko katika sera, sheria na kanuni ili kuimarisha usalama wa mifumo ya chakula, kuongeza bajeti ya serikali katika kilimo na kuelimisha wananchi.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja (kushoto) akimsikiliza Mkuu wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, Cosmas Ndakidemi (katikati) kuhusu bustani ya miche ya miti alipokuwa akikagua shamba la miti lililopo Manispaa ya Sumbawanga, mkoani Rukwa. Wengine ni watendaji kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini. (Picha na Wizara ya Utalii).

## Chamuriho: Wahandisi changamikieni miradi

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk Leonard Chamuriho amewataka wahandisi washauri kuchangamkia fursa zinazotolewa katika miradi ya kielelezo nchini ili kukuza taaluma zao na uchumi wa Taifa.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kitengo cha Mawasiliano Serikalini katika Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Chamuriho alitoa agizo hilo wakati akifungua Mkutano wa 35 wa Mwaka wa Wahandisi Washauri ulioandaliwa na Umoja wa Wahandisi Washauri (ACET), mkoani Dar es Salaam.

Alisema ni jukumu la wahandisi kuhakikisha miradi mikubwa ambayo ni ya kielelezo inatendewa kwa weledi na haki hasa kwa kuzingatia thamani ya fedha, ili kuleta tija kwa taifa na kuwawezesha kupata fursa zaidi katika miradi mingine inayotekelezwa nchini.

Aliwata wahandisi hao kuzingatia kuwa, sayansi na teknolojia vinakua kwa kasi, hivyo wahakikishe wanajijengea uwezo ili kuendana na kasi hiyo kwa kuhudhuria kozi mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Chamuriho alisema Serikali imeweka sera yenye mambo kadhaa makuu ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa upatikanaji wa masoko na kupiga chapuo katika wanye teknolojia ili kukuza wakandarasi wazawa.

Scanned with CamScanner

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi na Watu wenye ulemavu, Jenista Mhagama (katikati) akiwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kushoto), wakati wa kukagua eneo litakalofanyika uzinduzi wa mafunzo ya uanagenzi katika Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (MUST) juzi, kulia ni Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Aloyce Mvuma. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Wafugaji ng'ombe wa maziwa kunufaika bei

NIPASHE UK 16

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

MKUU wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vicent Anney, amewaahidi wafugaji wa ng'ombe wa maziwa kuanza kunufaika baada ya kuweka mikakati ya kutafuta wawekezaji ambao watanunua bidhaa hiyo kwa bei nzuri ukilinganisha na sasa, ambapo bei ya bidhaa hiyo sio ya kuridhisha.

Dk. Anney aliyasema hayo kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ambapo ziliibuka hoja mbalimbali kuhusu bidhaa hiyo kuuzwa kwa gharama ndogo, ukilinganisha na ubora wa bidhaa yenyewe.

Miongoni mwa mikakati ya Dk. Anney ni kukamilisha makubaliano ya mwekezaji ASAS pamoja na wadau wengine ambao wanaendelea kuvutiwa na mazingira mazuri ya wilaya hiyo.

"Lita moja ya maziwa huuzwa shilingi 600 na wanaonunua mfano Tanga Fresh wao huuza kwa shilingi 1,200 wakati uzalishaji wa maziwa wilayani Rungwe ni lita milioni 60 hii inaonyesha namna wafugaji wanavyopata hasara na bidhaa hiyo," alisema Dk. Anney.

Aliongeza kuwa hivi karibuni wataongeza ng'ombe wengine wa kisasa ili kuhakikisha bidhaa ya maziwa inapatikana kwa wingi na kutafuta soko la uhakika.

Kuhusu bei ya zao la kokoa, alisema serikali imetoa bei elekezi ya zao hilo ni shilingi 4,200 kwa kilo moja na sio vinginevyo na kuagiza kwa wanunuzi wote kuzungatia bei hiyo. Alisema hadi sasa baadhi ya maeneo wakulima wanalalamikia kukosa soko la kokoa kutokana na wanunuzi kutofika kwenye vyama vya ushirika, kutokana na tatizo hilo aliahidi kuongea na wawekezaji kuanzisha viwanda ili kuchakata zao hilo na kuongeza thamani ikiwamo utengenezaji wa chokleti.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Mpokigwa Mwankuga, alisema msimamo wa Baraza la Madiwani ni kuondoa walanguzi wote wanaowakandamiza wafugaji wa ng'ombe wa maziwa na kuendelea kuwashawishi wawekezaji wengine wenye nia ya kuwainua wafugaji.

Alisema baraza kwa kushirikiana na viongozi wa halmashauri wataendelea na jitihada za kuboresha mazingira ya upatikanaji na uzalishaji wa maziwa bora ili kupata soko la uhakika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Loema Peter, alisema bidhaa ya maziwa imekuwa na mchango mkubwa katika kuongeza mapato, na kwamba wataendelea kuboresha mazingira mazuri ili bei ya bidhaa hiyo iwe nzuri na kumnufaisha mfugaji.

Scanned with CamScanner

The Guardian

# Rungwe DC promises fair prices in milk production

By Guardian Correspondent, Rungwe

RUNGWE District Commissioner in Mbeya Region Dr Vincent Anney has promised dairy cows keepers that they will start reaping benefits following efforts to find investors who will buy milk at better prices than it is now.

Dr Anney made the remarks here at the weekend at the Rungwe District Council Councillors meeting in which various issues were raised in regard to low prices dairy keepers were getting from their high quality milk.

Among Dr Anney's strategies is to finalise agreement with Asas Dairy Company and other investors who have been wooed by the District's good environment in the dairy sector.

"A litre of milk is sold at 600/- and the buyer, say Tanga Fresh Company, sells at 1,200/- while the District's milk production is 60 million litres per year, which shows how dairy cows keepers are being shortchanged of their product," he said.

He added that they will soon add more modern dairy cows to make sure milk is obtained abundantly to meet the available market.

In regard to the cocoa crop, Dr Anney said the government has announced its indicative price - 4,200/- per kg and directed all buyers to abide by the price.

He said so far in some areas farmers are complaining for lack of the cocoa crop due to buyers not going to cooperatives societies, and promised to discuss with investors to establish cocoa processing factories including chocolate making.

For his part, Rungwe District Council Chairman, Mpokigwa Mwankuga said the Council's position is to remove all middlemen defrauding dairy cow keepers and urged other investors to come forward to assist them.

The Council's Executive Director, Loema Peter said dairy products has had great contribution in income generation and that they will continue to improve the environment to achieve higher prices to benefit keepers.

Scanned with CamScanner